ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

# TANGAZO KWA UMMA

## MABADILIKO YA KIWANGO CHA USAJILI WA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI

**Zanzibar, 7 Agosti, 2023**

### 1. UTANGULIZI:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inapenda kuujulisha Umma kwamba, kuanzia tarehe 1 Julai, 2023 kiwango cha usajili kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani kimebadilika kutoka Shilingi Milioni Hamsini **(TZS. 50,000,000)** na kuwa Shilingi Milioni Mia Moja **(TZS.100,000,000)** kwa mauzo ya kipindi cha miezi Kumi na Mbili (12).

Hii, ni kutokana na mabadiliko yaliyofanyika kwa mujibu wa **Kanuni ya 4 ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani za Mwaka 2012 chini ya vifungu vya 4, 15, na 69 vya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nambari. 7 2009**, ambayo inamtaka kila mfanyabiashara anaeuza bidhaa au kutoa huduma zinazopaswa kusajiliwa katika wigo wa kodi ya ongezeko la thamani anapaswa kwa kiwango hicho kuwa msajiliwa wa kodi ya ongezeko la thamani.

### 2. TARATIBU ZA USAJILI:

Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Kodi Ongezeko la Thamani za 2012, zinamtaka kila mfanyabiashara anaetoa huduma au kuuza bidhaa kujisajili katika wigo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa masharti yafuatayo:

2.1 Kwa mfanyabiashara ambae mauzo yake yanazidi au yanatarajiwa kuzidi Shilingi Milioni Mia Moja **(TZS 100,000,000.00)** kwa mwaka anawajibika kujisajili katika Kodi ya Ongezeko la Thamani ndani ya siku Thalathini (30) kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 3 na 4 ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani za Mwaka 2012.

2.2 Maombi ya usajili yatakapokamilika mfanyabiashara atapatiwa Cheti cha Usajili kutoka katika Ofisi za ZRA.

2.3 Kwa Mfanyabiashara aliyesajiliwa katika Kodi ya Ongezeko la thamani mwenye mauzo ambayo hayafikii kiwango cha Shilingi Milioni Mia Moja kwa mwaka **(TZS 100,000,000) anaweza kuomba kufutwa** katika usajili wa kodi hiyo kwa kuwasilisha Ritani ya Mwisho ya mauzo katika Ofisi za ZRA kama ilivyoainishwa katika **Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nambari. 7 ya mwaka 2009 kifungu cha 12.**

Mfanyabiashara ataondoshwa katika wigo wa kodi ya ongezeko la thamani baada ya kukidhi vigezo ikiwemo kufanyiwa uhakiki wa taarifa zake. Kwa mfanyabiashara atakaeondoshwa katika kodi ya ongezeko la thamani atajuulishwa kwa maandishi na kutakiwa kuwasilisha cheti cha awali cha Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika Ofisi za ZRA.

### 3. ATHARI YA KUTOKUWAJIBIKA:

Mfanyabiashara aliyetimiza vigezo vya kusajiliwa katika wigo wa kodi ya ongezeko la thamani na kushindwa kufanya maombi ya usajili, **itachukuliwa kuwa ameshasajiliwa kutoka siku ambayo alipaswa kusajiliwa** katika kodi hiyo kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nambari 7 ya mwaka 2009.

### 4. HITIMISHO:

Kutokana na marekebisho ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani za mwaka 2012 zilizoanza utekelezaji wake tarehe 1 Julai, 2023, ZRA inaahidi kusaidia kusimamia utekelezaji na uwajibikaji wa agizo hilo kwa mujibu wa Sheria kwa wafanyabiashara husika.

**"Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

Yusuph Juma Mwenda

**Kamishna Mkuu**